



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA SONGWE



TAREHE 25/01/2023

## TANGAZO LA KAZI YA MKATABA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Songwe anapenda kuwatangazia Watanzania wote wenye sifa na nia ya kufanya kazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Songwe kwa Mkataba wa muda kuomba nafasi zifuatazo:

### MSAIDIZI WA HESABU NAFASI – (4)

#### SIFA:

Awe na mojawapo ya sifa zilizotajwa hapa chini

- Aliyehitimu kidato cha IV na kufuzu kozi ya kozi ya Cheti cha ATEC level II au "Foundation Level" kinachotolewa na NBAA, waombaji wawe na uzoefu wa kazi zaidi ya mwaka mmoja (1) katika Fani hiyo.

#### KAZI NA MAJUKUMU:

- Kuandika na kutunza " Register" zinazohusu shughuli za Uhasibu.
- Kuandika hati za Malipo na hati za mapokezi ya Fedha.
- Kutunza Majalada yenye kumbukumbu za Hesabu.
- Kupeleka barua / nyaraka za Uhasibu benki.
- Kufanya usuluhisho wa masurufu, Karadha, Hesabu za Benki na Amana.

### NGAZI YA MSHAHARA TGS B MASHARTI YA JUMLA

- A. Mwombaji awe raia wa Tanzania ambaye ana umri si zaidi ya miaka 45
- B. Barua ya maombi iambatane na wasifu binafsi wa Mwombaji wa hivi karibuni (Curriculum Vitae)
- C. Barua ya maombi iambatanishwe na nakala ya vivuli vya vyeti vya kidato cha IV,VI, cheti cha kuzaliwa na vyeti vingine vya taaluma.
- D. Picha mbili ndogo (passport size) za hivi karibuni.

- E. Matokeo ya muda (provision/testimonials/statement of results) havitapokelewa.
- F. Waombaji wenye vyeti vya kidato cha nne na sita waliosoma nje ya nchi wanatakiwa kuwasilisha uthibitisho wa NECTA.
- G. Waombaji wenye vyeti vyeti vya Astashahada/ cheti vya nje ya nchi wanatakiwa kuambatanisha uthibitisho wa NACTE.
- H. Barua ya maombi iandikwe kwa lugha ya Kiswahili au kiingeleza.
- I. Mwisho wa kupokea maombi ni 01/02/2023 Saa tisa Alasiri.

Barua zote zitumwe kwa  
Mkurugenzi Mtendaji  
Halmashauri ya wilaya ya Songwe,  
S. L. P 77,  
Mkwajuni- Songwe.

**IMETOLEWA NA:**

Namnyaki Laitetei

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA YA SONGWE**

**MKURUGENZI MTENDAJI  
SONGWE**